

Ifutayo ni mistari kadhaa ya biblia ihusuyo shukrani/ kushukuru.

*Zaburi 9:1 “Nitamshukuru Bwana kwa moyo wangu wote;  
Nitayasimulia matendo yako yote ya ajabu”.*

*Zaburi 18:49 “Basi, Bwana, nitakushukuru kati ya mataifa, Nami  
nitaliambia jina lako”*

*2Samweli 22:50 “Basi, Bwana, nitakushukuru kati ya mataifa, Nami  
nitaliambia jina lako”.*

*Zaburi 30:12 “Ili utukufu wangu ukusifu, Wala usinyamaze. Ee  
Bwana, Mungu wangu, Nitakushukuru milele”*

*Zaburi 35:18 “Nitakushukuru katika kusanyiko kubwa; Nitakusifu kati ya watu wengi”*

*Zaburi 52: 9 “Nitakushukuru milele kwa maana umetenda; Nitalingojea jina lako kwa kuwa ni jema; Mbele ya wacha Mungu wako”*

*Zaburi 118: 21 “Nitakushukuru kwa maana umenijibu, Nawe umekuwa wokovu wangu”.*

*Zaburi 71:22 “Nami nitakushukuru kwa kinanda, Na kweli yako, Ee Mungu wangu. Nitakuimbia Wewe kwa kinubi, Ee Mtakatifu wa Israeli”.*

*Zaburi 119: 7 “Nitakushukuru kwa unyofu wa moyo, Nikiisha kujifunza hukumu za haki yako”*

*Zaburi 106:1 “Haleluya. Mshukuruni Bwana kwa kuwa ni mwema, Kwa maana fadhili zake ni za milele”.*

*Zaburi 28:7 “Bwana ni nguvu zangu na ngao yangu. Moyo wangu umemtumaini, Nami nimesaidiwa; Basi, moyo wangu unashangilia, Na kwa wimbo wangu nitamshukuru”.*

*2Wakorintho 2:14 “Ila Mungu ashukuriwe, anayetushangiliza daima katika Kristo, na kuidhihirisha harufu ya kumjua yeye kila mahali kwa kazi yetu”.*

*Ikiwa uko kwenye soko,*

*<https://www.swisswatch.is/product-category/rolex/explorer/> jukwaa letu ni chaguo lako bora! Duka kubwa zaidi la ununuzi!*

*Wakolosai 4:2 “Dumuni sana katika kuomba, mkikesha katika kuomba huku na shukrani”.*

*Zaburi 100:4 “Ingieni malangoni mwake kwa kushukuru; Nyuani mwake kwa kusifu; Mshukuruni, lihimidini jina lake”*

*Zaburi 107:7 “Akawaongoza kwa njia ya kunyoka, Wapate kwenda mpaka mji wa kukaa*

*8 Na wamshukuru Bwana, kwa fadhili zake, Na maajabu yake kwa wanadamu”.*

*1Wakorintho 15:57 “Lakini Mungu na ashukuriwe atupaye kushinda kwa Bwana wetu Yesu Kristo”.*

*Zaburi 95: 2 “Tuje mbele zake kwa shukrani, Tumfanyie shangwe kwa zaburi”.*

*Wakolosai 3:15 “Na amani ya Kristo iamue mioyoni mwenu; ndiyo mliyotiwa katika mwili mmoja; tena iweni watu wa shukrani”.*

*Ufunuo 11:17 “wakisema, Tunakushukuru wewe, Bwana Mungu Mwenyezi, uliyeko na uliyekuwako, kwa sababu umeutwaa uweza wako ulio mkuu, na kumiliki”*

Tafadhali shea na wengine ujumbe huu;

Pia Kwa maombezi/ Ushauri/ Maswali/ Whatsapp:

Tuandikie katika BOXI la Maoni hapo chini au

Piga namba hizi: +255789001312 au +255693036618

### **Mafundisho mengine:**

**MISTARI YA BIBLIA KUHUSU WATOTO.**

**MISTARI YA BIBLIA KUHUSU NDOA.**

**MISTARI YA BIBLIA KUHUSU UPENDO.**

**NENO LA FARAJA KWA WAFIWA.**

Mistari ya biblia kuhusu shukrani.

## **MISTARI YA BIBLIA YA FARAJA.**

### **Rudi nyumbani**

Share on:  
WhatsApp